# *MWONGOZO WA KUSAHIHISHA*

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**

**JULAI/AGOSTI 2025**

**KIDATO CHA PILI**

## SEHEMU YA (A)

### INSHA (Alama 15)

Wewe ni kiranja mkuu wa shule yenu, umealikwa katika mkutano wa wanafunzi na wazazi. Andika hotuba utakayotoa kuhusu elimu na nidhamu shuleni. (Alama 20)

Mambo muhimu:
(i) Kichwa
(ii) Utangulizi
(iii) Mwili
(iv) Hitimisho

## SEHEMU YA (B)

### UFAHAMU (Alama 20)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Mgomo wa madaktari ambao umekuwa katika taifa letu umesababisha madhara chungu mzima. Migomo mingi hutokea nchini na kuna haja ya suluhu la kudumu kupatikana ili kujiepusha na maafa yanayosababishwa na hali hii.

Migomo mingi inawaathiri walalahoi. Mgomo wa madaktari kwa mfano umekuwa na athari kubwa kwa walalahoi wanaotegemea hospitali za umma pekee kwa matibabu. Hata hivyo, baadhi ya hospitali hizi za umma hazina dawa za kutosa na pia wataalamu wa kutosha kushughulikia wagonjwa wanaofurika huku. Wasimamizi wengi wa hospitali hizi haawatilii maanani hali ya wagonjwa wanaofika pale kwani wakati mwingine tunasikia malalamishi kutoka kwa umma kuwa wagonjwa hawashughulikiwi kwa wakati uliofaa. Baadhi ya wauguzi haawashughulikii wagonjwa ipasavyo. Madaktari wengine pia wanawatibu wagonjwa lakini wanaelekeza wagonjwa kwenda kununua dawa katika maduka mengine huko nje. Wakati mwingine hakuna madaktari hospitalini kuwahudumia wagonjwa. Serikali ina jukumu kubwa kuhakikisha kuwa mgomo wa madaktari na wauguzi umeshughulikiwa ili kuridhisha pande zote, yaani wagonjwa na madaktari. Waonjwa wana haki ya mishahara mizuri kutokana na kazi au wajibu muhimu wanaotekeleza. Sharti serikali itimize makubaliano yake na madaktari. Ni haki ya madaktari pia kupata vifaa vifaavyo vya kufanyia kazi kama ilivyopendekezwa kwa mkataba wao wa awali. Viongozi wa serikali waliohusika kupitisha maafikiano hayo waitwe wawajibishwe na hawapaswi kushikilia nyadhifa yoyote uongozini.

Madaktari pia wanapaswa kuwaonea huruma baadhi ya wagonjwa wasiomudu kulipia matibabu katika hospitali za kibinafsi. Serikali inapasa kukumbuka kuwa uzalendo una mipaka na madaktari kama raiya wangine wana mahitaji ya kimisingi ya kugharamia.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## Maswali ya ufahamu

1. Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (Alama 1)

   ***Migomo na madhara yake***

2. Eleza mahila wanayopitia wagonjwa katika hospitali za umma. (Alama 4)

   ***a. Kutohudumiwa kwa waonjwa na madaktari hospitalini***
   ***b. Kutopata dawa baada ya kutibiwa hospitalini, wanatumwa kununua huko nje.***
   ***c. Wasimamizi wa hospitali hizi hawatilii maanani hali ya wagonjwa.***
   d. ***Ukosefu wa madaktari wa kuwahudumia wagonjwa***

3. Serikali ina jukumu lipi kwa taifa? (Alama 2)

   ***Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa mgomo wa madaktari umeshughulikiwa na kuwa pande zote zimeridhika.***

4. Madaktari wana haki gani kulingana na taarifa uliyosoma? (Alama 2)

   ***(i) Haki ya kupata vifaa vifaavyo vya kufanyia kazi***
   ***(ii) Haki ya mishahara mizuri***

5. Je, madaktari wana umuhimu gani katik taifa lolote? Toa amoni yako. (Alama 2)

   ***(i) Madaktari wana umuhimu wa kuwatibu wagonjwa wanaoenda hospitalini***
   ***(ii) Kuwashauri wagonjwa wanaogua maradhi mbalimbali***

6. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (Alama 4)
   a. Walalahoi - ***maskini***

   b. Wajibu – ***jukumu, jambo linalomlazimu mtu kulitimiza***

   c. Kugharamia – ***kushughulikia, toa fedha kwa ajili ya kitu***

   d. Kuridhisha **– *kutosheleza au kutosheka***

## SEHEMU YA (C) MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 25)

(a). Taja sauti mbili za midomo – meno. (Alama 2)

***(i) /f/***
***(ii) /v/***

***(b).*** Eleza maana ya sauti tatanishi. (Alama1)

***Ni sati ambazo zikitumika katika sentensi huleta hali ya mkanganyiko wa matamshi.***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(c). Mofimu ni nini? (Alama 1)
***Ni sehemu ndogo ya neno inayowasilisha maana kisarufi***

(d). Ainisha mofimu katika neno hili. (Alama 3)
Wanawalisha.
***Wa – mofimu nafsi/ngeli ya A – WA***
***Na – mofimu ya wakati uliopo***
***Wa – mofimu ya nafsi ya watendwa***
***L – mzizi***
***Ish – mofimu ya kauli/mnyambuliko***
***A – mofimu ya kiishio***

(e). Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi. (Alama 3)
Mwalimu angali mgonjwa hata kama amekuwa akifunza darasani.
***Angali – kitenzi kishirikishi kikamilifu***
***Amekuwa – kitenzi kisaidizi***
***Akifunza – kitenzi kikuu***

(f). Andika sentensi hizi kwa wingi. (Alama 2)
(i) Mtu yuyu huyu ndiye aliyeiba nguo yangu.
***Watu wawa hawa ndio walioba nguo zetu***

(ii) Nilinunua kitabu kiki hiki ulicho nacho'
***Tulinunua vitabu vivi hivi mlivyo navyo.***

(g). Yakinisha sentensi ifuatayo: (Alama 2)
Msomi hakutuzwa siku hiyo.
***Msomi alituzwa siku hiyo.***

(h). Tunga sentensi mbili kwa kutumia viwakilishivya nafsi huru na nafsi tegemezi. (Alama 2)
***Mimi naenda nyumbani (mimi – sisi – yeye –***
***Tuliondoka jana.***

(i). Andika kinyume cha sentensi hii. (Alama 1)
Hamisi alimwoa Farida mwaka jana.
***Hamisi alimtailki Farida mwaka jana***

(j). Nomino hizi ziko katika hali gani? (Alama 1)
(i) Kusoma
(ii) Chumvi

***Kusoma – ngeli ya KU – KU***
***Chumvi – ngeli ya I - I***

(k). Eleza maana mbili ya sentensi hii. (Alama 2)
Kamau alimpigia Otieno mpira
***(i) Kwa niaba ya Otieno***
***(ii) Kuelekea kwa Otieno***


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

***(iii)Kamau alimpiga Otieno kwa sababu ya mpira***
***(iv) Kamau alitumia mpira kumpiga Otieno***

(l). Eleza matumizi mawili ya kistari kifupi. (Alama 2)
***Kuonyesha silabi za neno (mwali-mu)***
***Kutenganisha silabi ili kuonyesha neno linaendelea***
***Kuandika tarehe 20-11-2024***
***Kutenganisha muda Fulani ( 1939-1945)***

(m). Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (Alama 1)
Ndege huyu ni dhaifu mno
***Kidege hiki ni kidhaifu mno***

(n). Taja aina mbili za sentensi. (Alama 2)
***(i) Sentensi sahili***
***(ii) Sentensi ambatano***
***(iii) Sentensi changamano/mseto***

## SEHEMU YA (D) ISIMU JAMII (ALAMA 5)

(i) Eleza sifa tano za sajili ya kituo cha polisi. (Alama 5)
- ***Lugha ya kudadisi***
- ***Luha huwa ya ukali mwingi***
- ***Lugha hurejelea sheria***
- ***Lugha legevu***
- ***Kuchanganya msimbo/ndimi***
- ***Lugha yenye heshima***
- ***Sentensi fupifupi***
- ***Lugha yenye vifupisho kwa wingi: mfano; OB.***

## SEHEMU YA (E) FASIHI SIMULIZI (ALAMA 5)

(i) Mtambaji ni nani? (Alama 1)
***Mtambaji ni msimulizi wa hadithi au huitwa fanani***

(ii) Eleza sifa nne za mtambaji bora. (Alama 4)
- ***Awe anaelewa hadithi yake***
- ***Awe anaelewa lugha ya hadithi yake***
- ***Awe mcheshi***
- ***Awe na ujuzi wa kusimulia***
- ***Awe na ujasiri***
- ***Awe na uwezo wa kuelewa utamaduni wa hadithi yake***
- ***Awe na ubunifu wa hali ya juu***
- ***Awe na uwezo wa kutumia viziada lugha***
- ***Aweze kutumia maleba yanayochukuana na kila anachosimulia***

Zozote nne Alama 4x1=4


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes